International Research Journal of Rongo University (IJORU) ISSN: 3005-7221
Transformative Research and Innovation for an Inclusive and Sustainable Future
Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

UKIUKAJI WA HAKI ZA WATOTO KWA MAENDELEO ENDELEVU: MFANO WA NOVELA YA KIVULI CHA MADHILA

[1]Nyandwaro K. Lena*, [1]Mark A. Odawo

*Corresponding Author: nyandwarolena@gmail.com

https://orcid.org/0000-0001-5236-359X; https://orcid.org/0009-0006-5602-4302

[1]Chuo Kikuu cha Rongo, Sanduku la Posta 103-40404 Rongo, Kenya

Ikisiri

Katiba ya Kenya (2010) inabainisha haki mbalimbali za watoto. Hata hivyo, haki za watoto bado zinakiukwa kutokana na madhila wanayopata katika jamii wanamokulia. Makala haya yanahakiki namna Malengo ya Maendeleo Endelevu ya jamii yanavyotingwa kutokana na kukiukwa kwa haki za watoto kama inavyosawiriwa katika novela ya Kivuli cha Madhila (Momanyi, 2023). Makala haya yaliyokitwa katika Nadharia ya Maadili yalichukua muundo elezi. Watafiti walibusisha usomaji wa kina wa novela husika ili kupata data yakini. Data ziliainishwa, kupangwa na kisha kuelezwa kupitia uchanganuzi wa yaliyomo. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kinathari. Utafiti huu ulibainisha kuwa watoto wananyimwa nafasi ya elimu, kufanyishwa kazi za sulubu, kupigwa, kuteswa, kutengwa na aila zao pamoja na kulanguliwa. Makala haya yanashikilia kwamba, ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yaweze kuhalisiwa kikamilifu kufikia mwaka wa 2030, ni muhimu haki za watoto zilindwe na wanajamii.

Maneno Muhimu: *Mtoto, Haki za Watoto, Ukiukaji wa Haki za Watoto, Maendeleo Endelevu*.

Utangulizi

Kwa mujibu wa United Nations (2015), Maendeleo Endelevu ni dhana inayorejelea maendeleo yanayotimiza mahitaji ya leo bila kuhatarisha uwezo wa vizazi vijavyo kutimiza mahitaji yao. Kulingana na Mwita na Odawo (2020), Malengo ya Maendeleo Endelevu ni matamanio ya ulimwengu yanayokusudiwa kuleta maendeleo ya kiuchumi, ujumuishwaji wa kijamii na uendelevu wa mazingira. Wanaendeleza kuwa, malengo haya yanaendeleza mafanikio ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia yaliyotekelezwa mwaka 2000-2015 ili kuhamasisha hatua za pamoja katika kuondoa umaskini na kutoa huduma za kimsingi za jamii na kufikia mwaka 2030. Umoja wa Mataifa (UN, 2015) huorodhesha Malengo ya Maendeleo Endelevu kumi na saba. Makala haya yamekitwa katika malengo matano yafuatayo yanayotingwa pale haki za watoto zinapokiukwa: Kuondoa dhuluma, kukomesha njaa, afya na ustawi, elimu bora pamoja na kazi zenye staha na ukuzaji uchumi.

Kulingana na Mulokozi (2017), Katiba ya Kenya (2010) na Sheria za Watoto (2022), mtoto ni mtu yeyote ambaye hajafikisha miaka kumi na minane. Katika Katiba ya Kenya (2010) Sura ya Nne, Kifungu cha Tatu, Ibara ya 53 inabainisha kuwa kila mtoto ana haki ya kuwa na utambulisho katika nchi alimozaliwa, haki ya kupata elimu, lishe bora, nyumba, matibabu, kulindwa kutokana na mateso na kupata malezi yanayofaa. Sheria ya Urithi (2015) Ibara 160 inaeleza kuwa, kila mtoto ana haki ya urithi. Kwa mujibu wa UNICEF-WHO (2020), kufikia 2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na watoto yanapaswa kuwa yameafikiwa. Malengo hayo ni kuwa: mtoto anastahili kulindwa kutokana na mateso na dhuluma ya aina yoyote, anakingwa kutokana na kazi za lazima na sulubu, ulaghai, unyonjaji, ulanguzi wa watoto na utumwa wa kisasa. Pia, mtoto anapaswa kupata elimu bora na ya bure kutoka shule ya chekechea hadi upili, lishe bora na maji safi, matibabu bora.

Takwimu za UNICEF (2024) zinaonesha kuwa watoto bilioni 1.6 duniani bado wanapitia aina mbalimbali za dhuluma ambazo huwa na athari hasi kwa afya yao ya kimwili na kiakili kadri wanavyoendelea kukua. Lengo 16.2 katika Malengo ya Maendeleo Endelevu linasema

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

kuwa dhuluma za aina zozote kwa watoto zinapaswa kukomeshwa kwa sababu hukiuka haki zao na kutinga utekelezaji wa malengo hayo. Pana haja ya jamii kuchukua hatua za kukabiliana na hali hiyo ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yaweze kuafikiwa kufikia mwaka wa 2030.

Njia mojawapo inayoweza kutumika kukomesha ukiukaji wa haki za watoto ni kuelimisha na kuhamasisha wanajamii kuhusu haki za watoto na kutoa mifano ya namna zinakiukwa katika jamii kupitia njia mbalimbali kama vile fasihi. Ripoti ya UNICEF (2024) inaeleza kuwa vyombo vya habari huchangia kwa kiasi kikubwa mchakato wa kuelimisha jamii kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu na masuala yanayohusiana na haki za watoto. UNESCO (2024) inasisitiza umuhimu wa kutumia hadithi kama njia bunifu ya kuwashirikisha wanajamii katika kufundisha Malengo ya Maendeleo Endelevu. Inafafanua kuwa, elimu inaweza kuwa ya darasani au sanaa na utamaduni. Fasihi kwa mujibu wa Mulokozi (2017) ni sanaa ya lugha iliyo na ubunifu inayoelezea kuhusu maisha, mahusiano, mazingira na hisia za binadamu katika mazingira anamokulia. Wamitila (2008) anaeleza kuwa dhima mojawapo ya fasihi ni kuhamasisha wanajamii ili wakosoe, wakemee, wadadisi na kupinga hali zinazodhalilisha kundi fulani la watu. Ogondo (2026) anaeleza kuwa maandishi ya fasihi ni muhimu katika kuelimisha jamii kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kwa hiyo, lengo la makala haya ni kuhakiki namna haki za watoto zinakiukwa na hivyo kulemaza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kurejelea novela ya *Kivuli cha Madhila*.

Kulingana na UNICEF-WHO (2020), Malengo ya Maendeleo Endelevu imetoa fursa maalum ya kuhakikisha kuwa haki za watoto zimelindwa na kuafikiwa na jamii kufikia mwaka wa 2030. UNHCHR (2017) inaeleza kuwa haki za watoto na Malengo ya Maendeleo Endelevu hutegemeana hivi kwamba malengo hayo hayawezi kuafikiwa bila kuzingatia utekelezaji wa haki za watoto. Hoja ya makala haya ni kuwa, ukiukaji wa haki za watoto ni njia ya kudumaza rasilimali muhimu inayotegemewa kwa kizazi cha kesho. Watoto wasipopata elimu, lishe bora na matibabu, basi, ukuaji wao utavyazwa na vipawa vyao kukosa kunolewa kwa ajili ya kutumiwa kuzalisha utajiri kwa taifa. Nguvu zao zinapofyonzwa kwa kufanyishwa kazi za sulubu zisizo na tija, na tabia zao kufisidiwa pale wanapolanguliwa, basi matarajio ya kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu ukuzaji wa maadili na upanuzi wa viwanda yatabakia kuwa ndoto.

Uhakiki wa Maandishi

Ogondo (2026) alihakiki tamthilia za Kiswahili ambazo ni: *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) na *Kodi* (Muhando, 2024) kama chombo cha kuhamasisha jamii kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Alibaini kuwa, tamthilia hizi zilikuwa na nafasi kubwa katika kuhamasisha jamii kuhusu malengo yafuatayo: Kukomesha njaa na umaskini, jinsia, ukuaji wa uchumi, miji na makazi endelevu pamoja na amani, haki na taasisi imara. Haya yalijitokeza kupitia migogoro na maamuzi ya wahusika. Japo utafiti wake natofautiana na wetu, hoja zake zinajenga makala haya yanayohakiki namna ukiukaji wa haki za watoto unavyolemaza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Matokeo ya utafiti wa Murimi na Mukuta (2024) kuhusu ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya za ya *Chozi la Heri* (Matei, 2017) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) yalibainisha kuwa, maamuzi na tabia za wahusika wengine zilichangia madhila kwa watoto. Utafiti wao unakaribiana na mawazo katika makala haya yaliyokuwa yanahakiki namna haki za watoto zimekiukwa. Hata hivyo kuna utafiti wetu umepiga hatua na kuangalia jinsi ukiukaji wa haki za watoto unavyolemaza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Katika utafiti wa Musindalo (2020) aliyehakiki haki za watoto katika riwaya za milenia mpya, ilibainika kuwa haki hizo zilikuwa na uhusiano mkubwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Huku utafiti wake ulijikita katika utanzu wa riwaya kuhakiki haki za watoto, makala haya yalihakiki ukiukaji wa haki za watoto unavyolemaza utekelezaji unaofaa wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kurejelea novela.

Msingi wa Nadharia

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Maadili iliyoasisiwa Martha Nussbaum (1983) na kuiendeleza mwaka wa 1995. Kulingana naye, maadili hufanya binadamu kuishi maisha yanayostahili. Anaeleza kuwa maadili ni sheria ambayo jamii imeweka kama vigezo vinavyofaa binadamu azingatie ili aishi maisha yanayostahiki. Posner (2009) anaeleza kuwa, nadharia hii inashikilia kauli kwamba kazi za fasihi hukakiki na kurekebsiha tabia na maisha ya

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

wanajamii na kuwafanya wawe watu bora. Plumer na Groake (2011) walihakiki insha za Nussbaum. Walibaini katika insha hizo kuwa haki ya kijamii na kisiasa hujitokeza katika kazi za fasihi zinazojenga taswira ya huruma, hali nzuri na mwisho unaofurahisha na kukubalika na wanajamii.

Mihimili ya nadharia hii ni: Mosi, kazi ya fasihi sio kuburudisha tu bali pia kuhakiki mema na maovu katika jamii. Pili, nadharia hii huhakiki mafunzo ya kimaadili yanayotolewa katika kazi husika na athari yake kwa jamii husika. Tatu, kazi za fasihi zinapaswa kuibua hisia za huruma kwa wasomaji wake. Mwisho, zinapaswa kuibua mijadala chanya katika maendeleo ya ploti yake na hadithi inapaswa kuaminika na kusawiri ulimwengu wa kihalisia.

Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kitaamuli. Ponera (2019) anaeleza kuwa, utafiti wa kitaamuli hutumia mbinu za kimaelezo katika kufafanua dhana, kutafuta suluhisho kwa tatizo au kuongeza maarifa kuhusu jambo fulani. Katika makala haya, novela ya *Kivuli cha Madhila* ilihakikiwa kwa lengo la kuonesha namna haki za watoto zimekiukwa na kulemaza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika katika kuteua novela ya *Kivuli cha Madhila*. Creswell na Poth (2024) wanaeleza katika usampulishaji huu, mtafiti huteua vitu au washiriki kimaksudi kutokana na sifa au taarifa walizonazo ambazo zitampa data anayohitaji katika utafiti wake. Licha ya kutoa data zilizofanikisha mahitaji ya utafiti huu, novela ya *Kivuli cha Madhila* iliteuliwa kutokana na utanzu huu kuingizwa katika Mtaala wa Elimu ya Umilisi (CBE) uliotangulizwa nchini Kenya mwaka 2017. Wasomi wengi sasa wameanza kuchanagamkia utanzu huu kwani inaangazia masuala muhimu yanayoathiri jamii.

Katika utafiti huu, data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa novela husika kisha ziliainishwa, kupangwa na kisha kuelezwa kupitia uchanganuzi wa yaliyomo. Ogechi (2024) anaeleza kuwa katika uchanganuzi wa data, mtafiti hutoa maelezo yanayoambatana na madhumuni ya utafiti wake na hujikita katika mihimili ya nadharia inayoongoza utafiti huo. Kulingana na Krippendorff (2018) uchanganuzi wa yaliyomo huhusiha huhakiki wa yaliyomo kwenye maandishi kwa lengo la kubaini maana, dhamira, malengo na ujumbe uliomo kwenye kazi husika. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya Nadharia ya Uhakiki wa Maadili ili kuoonesha haki za watoto zilivyokiukwa na kulemaza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Matokeo ya Utafiti

Baadhi ya wahusika katika novela ya *Kivuli cha Madhila* ni watoto na vijana ambao wanapitia madhila mbalimbali mikononi mwa walezi wao na watu wengine. Madhila haya yanakiuka haki zao kama watoto na hivyo kulemaza utekelezaji faafu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Wahusika watoto na vijana hawa ni: Kalinge, ambaye ni mtoto yatima anayelazimika kuishi kwa ami yake Bwana Masuji na mkewe Bi. Nanai mjini Mapitano baada ya wazazi wake kufariki kwa mafuriko. Mtoto mwingine ni Mtumwa anayeishi na shangazi yake. Anapitia mateso mengi mikononi mwa shangaziye hali inayomfanya atoroke. Anaamua kutafuta ajira na anapata kwa duka la bwenyenye mmoja. Kuna watoto wavulana pamoja na kijana Mbanda ambao ni wafanyakazi katika kinu cha pamba kinachomilikiwa na Bwana Fedha na wenzake kama Bwana Masuji na mhindi Nanji. Kinu hiki cha pamba kimepewa jina fiche la Cotton Estate Academy ili kuficha maovu wanayotendea watoto. Saidi ni kijana ambaye ameacha shule na anafanya kibarua katika gereji ya mhindi Nanji.

Kulingana na Nadharia ya Uhakiki wa Maadili (Nussbaum, 1983), kazi ya fasihi inapaswa kumulika mema na maovu katika jamii. Makala haya yalichukulia madhila wanayopitia watoto na vijana kuwa maovu yenye utovu wa maadili. Pia, makala haya yalizingatia mhimili kuwa kazi ya fasihi inapaswa kusawiri ulimwengu halisia wa binadamu. Katika kuhakiki namna haki za watoto zinavyokiukwa, makala haya yalijikita katika takwimu za UNICEF (2024) kuwa kuna watoto katika ulimwengu wa kihalisia wanaopitia madhila haya. Pia uhalisia ulijitokeza katika kunasibisha ukiukaji wa haki za watoto katika novela ya *Kivuli cha Madhila* na namna inavyolemaza Malengo ya Maendeleo Endelevu. Alfarhan (2024) anaeleza kuwa fasihi husawiri maisha ya wanajamii, yale wamezoea kufanya na uhalisia wa jamii zao. Katika novela ya *Kivuli cha Madhilia* haki za watoto zimekiukwa kwa njia zifuatazo:

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

Kunyimwa Nafasi ya Kupata Elimu

Kwa mujibu wa Al-Shuaibi (2014), elimu ni mchakato wa kupata maarifa na kujenga ubunifu kwa madhumuni ya kuimarisha maisha ya baadaye ya mtu na kuboresha mahusiano yake na wengine. Asasi ya elimu ina nafasi kubwa katika kufinyanga jamii ili kufikia malengo yake ya kiuchumi na kutatua changamoto za kimaadili (Ngatia na wenzake, 2020). Kasuma na Odawo (2025) wanahoji kuwa elimu hudhamiria kujenga akili, tabia na uwezo wa mtu binafsi kwa kupitisha maarifa, ujuzi na maadili ili kuwaandaa wanajamii katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Kulingana nao, elimu hufanikisha haya kwa kutekenya mielekeo na mienendo ya wanajamii ili kulandana na matarajio ya jamii husika na kwa kuwarithisha vijana mikakati ya kuwawezesha kupambana na changamoto za maisha kama vile ukosefu wa ajira. Situma na Wasike (2020), wanashadidi mawazo haya kwa kueleza kuwa lengo la elimu ya juu ni kumpa mwanafunzi maarifa amilifu ili kumwezesha kuchangia katika maendeleo ya jamii yake.

Al-Shuaibi (2014) anaeleza kuwa elimu ni asasi yenye dhima ya kupanua mwonoulimwengu wa wanajamii na kuwapa uwezo wa kupambana na maovu kama vile ukandamizaji na ufisadi. Mbali na manufaa ya kiuchumi, maarifa yanayotokana na elimu huwa nguzo muhimu ya kupanua ujuzi wa kutatua migogoro kati ya watu na hivyo kuhakikisha mshikamano na muumano katika jamii (Meyer, 1977). Kiumi na Chiuri (2005) na Ndiku (2007) wanaafikiana kuwa elimu ni zana muhimu ya kukuza rasilmali miongoni mwa binadamu wanaoitumiwa kuleta maendeleo katika nchi.

Katika novela ya *Kivuli cha Maisha*, Kalinge ananyimwa haki ya kuendelea kusoma. Alipokuwa kwao kijijini Mwembekoko, wazazi wake walijukumika na kumpeleka shuleni. Alikuwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule ya upili ya Magangao (uk.21). Baada ya wazazi wake kuaga dunia, anahamia kwa ami yake Bwana Masuji, mjini Mapitano. Kalinge anapomuuliza ami yake iwapo atamtafutia shule ili aweze kuendelea na masomo yake, anamweleza kuwa haoni haja ya yeye kuendelea na masomo. Katika uk. 8 na 9, mwandishi anatueleza kuwa kila alipomkumbusha Bwana Masuji kuhusu suala la shule, alitoa vijisababu kama vile hajapata shule nzuri, hana karo na alimkumbusha kuwa mwanaume ni kutafuta na kuchuma mali kwani wapo wengi ambao walimaliza kusoma lakini hawana ajira. Bwana Masuji anasema katika uk. 45 *"…basi nasema hivi, shule huendi na hutaenda bila idhini yangu. Wewe si mtoto wa kike kwamba utaolewa. Lazima ujifunze kazi za mikono, ujue kulima, kulisha mifugo na kutafuta pesa."*

Katika uk.11, mgema mmoja ambaye anafanya kazi kwa shamba la Bwana Masuji anamkejeli Kalinge kuwa mabuku hayana maana siku hizi. Pia ukurasa huo huo, mwandishi anatueleza kuwa alienda kwa shangazi yake Bi. Nanai kumrai ikiwa ataongea na mume wake ambaye ni ami yake Kalinge ikiwa atamrudisha shule. Anamfokea na kumwambia asahau azma ya kurudi shuleni na kwamba ana bahati ana pahali pa kulala na chakula cha kula kwani wapo watoto wengi ambao hawana bahati ya kupata makao na chakula. Kupitia maelezo ya Mtumwa kwa Mkuu wa Polisi katika uk. 113, inabainika kuwa shangazi yake hakumpeleka shule baada ya wazazi wake kuaga dunia. Hali hii inamnyima Mtumwa haki yake ya kusoma.

Kwa mujibu wa ripoti ya UNCRC (1989) kifungu cha 28, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu ya msingi inapaswa kuwa ya bure na mtoto huyo anapaswa kupata elimu ya sekondari pia. Kifungu cha 29 kinasema kuwa lengo la elimu linapaswa kukuza hulka, talanta ya mtoto na kumhimiza kuwaheshimu watoto wenzake, wazazi, mazingira na tamaduni zao. Pia Katiba ya Kenya (2010) kifungu cha nne kinaeleza kuwa kila mtoto ana haki ya kupata elimu bora. Anayoyapitia Kalinge mikononi mwa ami yake, shangazi yake na maneno ya mgema yanalemaza lengo la nne la Maendeleo Endelevu linayosema kuwa kufikia mwaka wa 2030, watoto wote wanapaswa kupata elimu ya ubora na usawa ili maisha yao yaye bora. (UNICEF, 2024).

Kulingana na UNCRC (1989) kipengele cha 17, kila mtoto ana haki ya kupata maarifa inayofaa na ambayo itaendeleza ukuaji wake kwa njia chanya. Hali ni kinyume katika *Kivuli cha Madhila* kwani katika uk. 46, Kalinge anashangaa maelezo hasi ya babake mdogo Bwana Masuji kuwa elimu si ya maana. Anayafananisha mawazo hayo na mawazo ya baadhi ya wazazi kwa watoto wao. Anawaza *"…wazazi kama Masuji ndio wanaowaharibu watoto wao kwa kuwaonyesha pesa kuliko kuwafunza namna ya kuwajibika ili wazipate."* Pia, watoto wanapaswa

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

kulelewa katika mazingira ya kuwatia moyo kuhusu umuhimu wa elimu na wana haki ya kupata ajira pindi wanapomaliza shule.

Hali hii imelemaza utekelezaji wa Lengo la nne ya Maendeleo Endelevu inayosisitiza kuwa ni muhimu watoto wapate elimu bora na nasaha kutoka kwa watu wazima ambayo itawasaidia kuwa binadamu ambao wamejukumika. Baadhi ya watoto wamekata tamaa na kuacha shule kwa sababu wanaona wengi ambao wamesoma hawajapata ajira. Katika uk. 57, Saidi anamweleza Kalinge, *"Hata ukisoma, kazi ziko wapi? Wenzetu waliosoma bado wanahangaika kusaka kazi ambazo hazipo. I say, ya nini kupoteza muda wangu ikiwa nitafanya kazi na kupata pesa zangu mwenyewe bila masharti?"* Watoto hawa wanaona ni heri kufanya kazi ya kijungu jiko ili wakimu mahitaji yao. Saidi anafanya kazi kwe gereji ya Mhindi Nanji badala ya kusoma. Hali hii ya watoto kusoma na kukosa ajira inalemaza dhana ya watoto kuwa na maisha bora baada ya kusoma katika Lengo la Maendeleo Endelevu linaloshughulikia elimu. Kupitia elimu, ni haki ya kila mtoto kupata maelekezo yanayofaa kuhusu maisha. Nadharia ya Uhakiki wa Maadili inaeleza kuwa fasihi inapaswa kumulika maovu na mema katika kazi husika. Masuji, Nanai na Mgema kumnyima Kalinge fursa ya kuendelea na masomo na kukejeli azma yake ya kupata elimu mtawalia ni tendo ovu.

Kufanyishwa Kazi za Sulubu

Kazi ya sulubu, kulingana na Sennet (2008) ni kazi inayofanywa na binadamu kwa kutumia nguvu nyingi kupindukia nguvu zake za kawaida. Anatoa mifano ya kazi za sulubu kama vile ya ujenzi wa nyumba, kilimo, kuchimba migodi na kazi ya viwandani. Kwa mujibu wa UNICEF (2020), watoto wanaohusishwa katika kazi za sulubu, ukuaji wao na hali yao kwa kijumla huathirika kwa njia hasi. Kalinge anafanyishwa kazi za sulubu na Bwana Masuji. Katika uk. 9 na 10, mwandishi anatueleza kuwa, *"…tangu kuwasili nyumbani kwa Masuji, Kalinge alikuwa akitumikishwa katika mabanda ya kuku; awalishe, awape dawa, akusanye mayai na kuyapeleka kwa wateja kila asubuhi…alihitaji kufagia mazizi ya ng'ombe na ndama kisha ajiunge na vibarua kupalilia shamba au kukusanya mazao kama vile nazi, machungwa, ndimu, malimau na maembe…aliyajaza mazao kwenye vipeto na kuyapakia kwa magari ya wachuuzi."* Pia katika uk. 36, Bwana Masuji anamwelekeza kuwa itakuwa jukumu lake kuhakikisha kuwa mabanda ya kuku na mabata wanaishi katika mazingira yanayofaa kwa kufagia mabanda hayo, kuawa ndege hao dawa na kuwalisha mara mbili kwa siku. Isitoshe, alitarajiwa kuokota mayai na kuyapeleka kwa wateja kila asubuhi.

Watoto katika kinu cha pamba wamechukuliwa kama watumwa na wanatumikishwa kufanya kazi nyingi. Katika uk. 61, Kalinge anashangaa kuona kuwa wafanyakazi walikuwa watoto wavulana wenye umri wa wa miaka kumi na vijana wa rika lake. Kutokana na kazi ngumu ambao watoto hao walifanyishwa, nyuso zao zinaonekana kusinya, waliota vipele na ngozi zao zilikuwa zimeparara. Aransiola na Justus (2018) wanaeleza kuwa kazi za sulubu hudhibiti ukuaji wa watoto kiafya, huathiri akili zao na huwapa msongo wa mawazo. Pia, kulingana na Briceno na Pinzon (2004), kazi za sulubu huwapa watoto majeraha, magonjwa na huwafanya kuchoka. Katika kifungu cha 32 (UNCRC, 1989), kila mtoto anapaswa kulindwa kutokana na unyanyasaji wa kiuchumi na kufanyishwa kazi ngumu ambayo itaathiri afya yao kwa njia hasi na kulemaza uwezo wao wa kuendelea na masomo.

Katika uk. 64, mwandishi anaeleza kuwa kazi ya watoto wavulana kwenye kinu cha pamba ilikuwa ni kuchambua pamba, kuanika juani na kupakia marobota kwenye magari kila siku kuanzia saa moja za asubui kila siku isipokuwa siku ya Jumapili. Hali hii inaashiria kuwa vijana hawa walifanyishwa kazi ngumu siku nzima. Katika uk. 89, Kalinge anafanyishwa kazi ya sulubu na watu ambao walimteka nyara. Mwandishi anatueleza kuwa aliamshwa asubuhi kwa fujo, akapewa nguo kuukuu avae na kuoneshwa rundo la vyombo vichafu na nguo chafu ambavyo alitarajiwa aoshe. Kabla ya kumaliza kazi ya kuosha, aliamrishwa apike chai na kufua zulia nzito ambalo alishindwa kulifua kutokana na uzito wake. Mwandishi anatueleza kuwa *"…siku hiyo, Kalinge alishinda akiamrishwa na kukemewa mithili ya mtumwa. Ashike hili, mara aashiriwe aache ashike jingine. Hakupata nafasi ya kuonja kisebeho usiseme kupiga mswaki! Kadhia zilikuwa nyingi za kumtia udhia."*

Mtumwa katika masimulizi yake (uk. 111) anaeleza hivi *"…nilikuwa nikitumika kama mtwana katika duka la bwanyenye mmoja…huyu alinizidishia*

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

uchungu…" Anayoyapitia Mtumwa inakiuka haki yake ya kulindwa kutokana na kazi ya sulubu. Hali wanamojikuta Kalinge, Mbanda, watoto wavulana katika kinu cha pamba na Mtumwa ya kufanyishwa kazi nyingi na ngumu, inakiuka Lengo la nane katika Maendeleo Endelevu inayosisitiza kupigwa marufuku kutumikisha watoto kazi ngumu na ya sulubu. Watoto wengi katika ulimwengu wa kihalisia wamejipata wakifanya kazi ya sulubu na kutumikishwa pasi na hiari yao na watu wazima. Hili kulingana na Nadharia ya Uhakiki wa Maadli ni tendo baya, kwani haki yao imekiukwa.

Kunyimwa Haki ya Urithi

Wangai (2024) anaeleza kuwa kuwa urithi ni mfumo wa familia wa kupitisha mali kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ishaku na Abimbola (2024) wanaeleza kwamba urithi ni mchakato wa kurithisha mali kwa mrithi baada ya kifo cha mmliki wa mali husika. Mmliki anaweza kuwa mzazi, mlezi au msamaria mema. Mchakato huu unatambuliwa kisheria. Sheria ya Urithi Ibara 160, inasema kuwa kila mtoto pasi na kuzingatia jinsia yake wala kuzaliwa kwake ndani au nje ya ndoa au ni kuasiliwa ana haki ya urithi kutoka kwa wazazi wake.

Mwandishi wa *Kivuli cha Madhila* katika uk. 51, anatueleza kuwa Kalinge alikuwa na hamu ya kutembelea kaburi la wazazi wake kwa shamba lao kule kijijini Mwembekoko. Alipofika pale, alikutana na hali ya kutamausha alipokutana na bawabu amabaye alikuwa mlinzi wa shamba hilo. Alimweleza kuwa shamba hilo halikuwa lake tena kwani liliuzwa na Bwana Masuji kitambo kidogo. Uuzaji wa shamba ni jambo ambalo Bwana Masuji hakumuuliza wala kumwaarifu Kalinge licha ya yeye kuwa na haki ya kufahamu kwa sababu ulikuwa urithi kutoka kwa wazazi wake. Hali hii inamtamausha na anaonekana akirudi kwa Bwana Masuji akiwa msongo wa mawazo. Anajizungumzia hivi: *"…Ba…mdogo…kwa nini unipokonye hata kilicho changu? Urithi wangu umenipoka…machozi yalianza kumtiririka…machozi yakalowesha shati alilovaa…"* (Uk. 52). Hali anayopitia Kalinge imeshadidiwa na utafiti wa Frankline na wenzake (2026) ambaye anaeleza kuwa ukiukaji wa haki ya urithi humsababishia binadamu msongo wa mawazo, upweke, huharibu mahusiano ya kifamilia na kuteseka kwa muda mrefu. Hali hii ya Bwana Masuji kuuza shamba la wazazi wake ambalo lilikuwa urithi wake linamkasirisha Kalinge na katika uk. 52, anakata shauri ya kuhana kutoka kwa Bwana Masuji. Kutokana na haya, Kalinge anakosa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi kupitia miradi ya ukulima kwa kupokonywa shamaba.

Katika uk. 66, watoto wanaokamatwa na kupelekwa kufanya kazi kwa kinu cha pamba ni wale wanaoishi mitaani kwa sababu hawana urithi wala wanakoita nyumbani. Hali ya Kalinge na waatoto wavulana wa mitaani ambao hawana urithi inalemaza Lengo la kwanza la Maendeleo Endelevu linalosema kuwa kufikia mwaka wa 2030, mataifa yanapaswa kuhakikisha kuwa wananchi wake si maskini, wanafikia malighafi ya kiuchumi kwa hali sawa na wanamiliki shamba na rasilimali.

Kukosa Lishe Bora

Siu na Drewnowski (2003) wanaeleza maana ya lishe bora kuwa ni hali ya binadamu kula chakula kilicho na virutubisho muhimu kwa kiwango kinachofaa kwa lengo la kuboresha afya yake. Kwa mujibu wa UNRC (1989), kipengele cha 24, kila mtoto ana haki ya kupata lishe bora ili aweze kukua vyema. Ziegler (2001) ana maoni sawa na ya UNESCO (1999), kuwa kila binadamu ana haki ya kupata chakula bora, kila wakati, siku zote bila udhibiti wowote ili aweze kuishi maisha bora na yenye hadhi. Katika *Kivuli cha Madhila*, uk. 44, mwandishi anatueleza kuwa *"…pale nyumbani, alikuwa (Kalinge) anapitia masimbulio na karaha nyingi huku chakula kikiwa ni cha mshindio tu…"* Kalinge hapati chakula cha kutosha kwa ami yake licha ya kufanya kazi nyingi na ngumu. Kulingana na UNCF (2004), kila mtoto ana haki ya kupata chakula bora na cha kutosha ambacho kitamwezesha kuishi na kukua kiafya. Maelezo haya yanalandana na maelezo ya Sheria ya Watoto (2022) ambayo inasema kuwa ni haki ya kila mtoto kupata chakula cha kutosha na bora ili aweze kukua wakiwa na afya njema. Kulingana na Lengo la pili katika Maendeleo Endelevu linalohusu watoto kupata chakula bora na cha kutosha linalemazwa kupitia Kalinge kunyimwa chakula cha kutosha. Ni hali ambayo watoto wengi katika ulimwengu wa kihalisia wanapitia. Hali ya Kalinge kupata chakula kidogo sana licha ya kazi nyingi anayofanya ni tendo linalokiuka maadili ya kibinadamu.

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

Ukosefu wa Makazi Bora

Kwa mujibu wa Shirika la UN-Habitat Agenda (1996), makazi bora ni yale yanayompa binadamu usiri, usalama, nafasi ya kutosha ya kufanya shughuli za nyumbani, ina mwangaza wa kutosha, maji safi na hewa safi. Thiele (2002) anaongezea kuwa makazi bora yanapaswa kuwa na amani, ulinzi bora dhihi ya wahalifu pamoja na mabadiliko ya hali ya anga. Kulingana na UNCRC (1989) kipengele cha 27, ni haki ya kila mtoto kupewa makazi bora na walezi wake. Katika *Kivuli cha Madhila*, haki ya Kalinge ya kupewa makazi ya hadhi inakiukwa na Bwana Masuji. Katika uk. 1, mwandishi anaeleza kuwa *"…kitanda alichokilalia ni kibovu na kilipiga mayowe, chumba chake kilikuwa ghala ya makorokoro, makao ya panya, mende, mijusi, popo na ng'ende. Pia chumba hicho kilikuwa na nyufa nyingi ukutani."* Katika uk. 42, Kalinge anashangaa kwa nini ami yake alimpa chumba kibovu kilicho nje ilhali alikuwa na jumba lililo na vyumba vikubwa na vizuri. Pia, alipopelekwa kwa kinu cha pamba na mhindi Nanji katika uk. 64, Kalinge anakakikagua kijumba alichopewa na kukilinganisha na jela.

Haki ya Kalinge na wavulana ambao wanafanya kazi katika kinu cha pamba ya kupewa makazi bora inakiukwa na kulemaza Lengo la kumi na moja la Maendeleo Endelevu ambalo linaeleza kuwa kufikia mwaka wa 2030, kila binadamu akiwemo aliye na mahitaji maalum kutokana na ulemavu wa aina yoyote anapaswa kuwa anaishi kwa makazi ambayo anaweza kugharamia, iliyo na usalama na inayotosha. Katiba ya Kenya (2010) kipengele cha 21 Ibara ya Tatu inatambua watoto kuwa katika kategoria ya binadamu walio na mahitaji maalum na kipengele cha 56 kinasema kuwa kila mtoto ana haki ya kuwa na malazi bora.

Dhuluma ya Kisaikolojia

Cappa (2023) anaeleza kuwa dhuluma kwa watoto ni matendo yenye kukosa maadili ambayo wanatendewa kimaksudi ili huwadhuru kimwili, kisaikolojia na wakati mwingine huwasababishia kifo. Kulingana na WHO (2026) dhuluma kwa watoto ni unyanyasaji wa watu walio chini ya miaka 18 ambao huendelezwa na wazazi, walezi, watu wasiowajua, wapenzi na watoto wenzao. Kimataifa, imekadiriwa kuwa watoto zaidi ya bilioni moja wenye umri kati ya miaka 2-17 wamepitia au wanapitia dhuluma mikononi mwa wazazi, walezi wao, watoto wenzao, watu wasiowajua ama marafiki wao. Kwa mujibu wa WHO (2026) aina za dhuluma kwa watoto ni: dhuluma ya kisaikolojia, dhuluma ya kimwili, dhuluma ya kingono, udhalilishaji, kuteswa na unyanyasaji/uonevu, ulanguzi wa watu na utumwa wa kisasa. Katika *Kivuli cha Madhila*, mwandishi anatusawiria jinsi watoto wamedhulumiwa kisaikolojia.

Doherty na Berglund (2008) wanaeleza kuwa dhuluma ya kisaikolojia inahusu kumtisha mtu, kumfedhesha, kumtenga na kumtelekeza. Kulingana na Ungvarsky (2024) dhuluma ya kisaikolojia hudhuru akili. Binadamu ambaye anaendeleza dhuluma hii hutumia maneno, ishara na matendo makali kwa mwathiriwa. Anaeleza kuwadhuluma hii hudhihirika sana miongoni mwa wanajamii ikilinganishwa na dhuluma zingine. Ferrara na wenzake (2019) wanaeleza kuwa pana haja ya kutafiti dhuluma ya kisaikolojia miongoni mwa watoto katika kazi za kiusomi kwa sababu haijashughulikiwa kwa mapana, jambo ambalo makala haya yaliangazia katika novela ya *Kivuli cha Madhila*.

Dhuluma hii inajitokeza kwa njia mbalimbali kupitia watoto. Bwana Masuji na Bi. Nanai wanendeleza dhuluma ya kisaikolojia kwa Kalinge wanapomnyima fursa ya kwenda shuleni. Katika uk. 47, mwandishi anatueleza hali ambayo alikuwepo baada ya kunyimwa nafasi ya kwenda shuleni. Mwandishi anaeleza kuwa *"kichwa kilimuwanga (Kalinge)…akafuuza hadi chumbani mwake na kujibwaga kitandani…alihisi kama mtumwa…wazo la kuwa yeye ni mtumwa lilimtafishi, likamtia majonzi…"* Kalinge anatekwa nyara na watu ambao hawajui (uk. 81). Wanamwingiza kwenye buti la gari aina ya Probox. Akiwa mle ndani, mwandishi anatueleza kuwa *"…alianza kujiburumia…wahaka ukamvaa ukamfanya kuhisi kisunzi na matumbo kuchezacheza…alisalia mle akiomba Mungu wake huku machozi yakimtiririka..."* Uoga ambao anapitia unaashiria dhuluma ya kisaikolojia ambao umesababishwa na watu ambao walimteka nyara kwani hana ufahamu wa watu wale wala anakopelekwa.

Kalinge anapitia dhuluma ya kisaikolojia kupitia unafiki wa watekaji nyara ambao siku ya kwanza walimkaribisha vizuri, kumpa chakula na pahala pazuri pa kulala. Hali inabadilika asubuhi wakati wanamwamsha kwa fujo na kumpa kazi nyingi na ya

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

sulubu kufanya. Mwandishi anaeleza kuwa, *"mtu yule aliyekenua meno jana usiku na kumpigia magoti ale chakula, sasa alikuwa mkali kama simba…alishangaa kama kweli huyu ndiye yule aliyejinyenyekeza kwake akimsihi ale chakula…"* (kur. 89-90). Mmoja wao anamkazia macho, na kumwonesha ishara ya kumchinja shingo hali iliyomwogofya Kalinge ambaye anahisi maisha yake yamo hatarini na ishara hiyo inamkumbusha panga ambazo aliziona wakinoa (uk. 90). Katika uk. 92, mmoja wa watekaji nyara anamletea bata mzinga amchinje na kumpika. Mwandishi anatueleza kuwa alikuwa bata mzinga mkubwa na Kalinge anaogopa kwani ni mara yake ya kwanza kuamrishwa kumchinja na kutayarisha kitoweo kama hicho. Hali inamtia uoga na wasiwasi akilini mwake akihofia kuchinjwa alivyomchinja bata mzinga.

Kadhalika, Kalinge anakumbana na dhuluma ya kisaikolojia anapotoroka kwa watekaji nyara na kujipata mjini ambapo anafumaniwa na Kadio ambaye alikuwa mfanyakazi wa ami yake. Katika harakati ya kutoroka, anatuhumiwa kuwa mwizi na hapo anashikwa na polisi na kupelekwa gerezani. Akiwa ndani ya gari, polisi anamwambia maneno makali kama vile, *"…utasema huko mbele, kijana. Nyie ndio mnachafua jina la mji huu. Vibaka nyie!"* (uk.109). Anapolia kutokana na woga, polisi mmoja anamtisha kwa kumwonesha mtutu wa bunduki huku akimtupia maneno makali. Anamwambia katika uk. 110 *"…nitakunyamazisha usipofunga hilo pango lako la maneno."* Maneno haya yanamwogofya Kalinge na anaishia kufyata mdomo wake. Mle gerezani, anapatana na mtoto ambaye anaitwa Mtumwa. Mtoto huyu naye amepitia dhuluma ya kisaikolojia mikononi mwa shangazi yake. Anaamua kutoroka na kupata kazi kwa bwanyenye ambaye pia alimtuhumu kuwa mwizi. Kutokana na tuhuma zisizo na msingi, anajipata gerezani ambapo anaonekana kusononeka na kulia sana, hali inayoashiria amedhulumika kisaikolojia.

Pia, jina la mtoto huyu, yaani Mtumwa, ni jina ambalo maana yake linaweza kumsababishia madhila na kuendeleza dhuluma ya kisaikolojia kutoka kwa wanajamii. Wakiwa gerezani, katika uk. 113, kabla ya kuagana na Kalinge, anamshauri hivi: *"…jina hilo linaleta adha kwa yeyote aishiye leo na kero moyoni. Lifute kabisa katika nafsi yako ujiepushe nuksi na udhia kutoka kwa watu."* Kulingana na Katiba ya Kenya (2010) na Tume ya Mageuzi ya Sheria Nchini Kenya (KLRC, 2022) kipengele cha 53.1, kila mtoto ana haki ya kupewa jina pindi tu anapozaliwa. Pia, kipengele 53.2 kinasema kuwa maslahi bora kwa mtoto ni jambo la msingi ambalo linapaswa kuzingatiwa wakati uamuzi wowote ambao unamlenga mtoto. Njia mojawapo ya kuhakikisha maslahi yake ni bora ni walezi kuwapa mtoto jina ambalo lina maana faafu au la kimaadili. Kwa hiyo, sadfa ya maana ya jina lake na madhila anayoyapitia ni tukio linalomtinga kisaikolojia na hivyo kukiuka haki zake.

Mfano mwingine wa dhuluma ya kisaikolojia ni katika kur. 130-132 ambapo Kalinge anaombwa na Saidi kumsaidia kubeba vipuri vya gari. Hamwelezi kuwa ni mali ya wizi na kwa bahati mbaya wanashikwa. Kalinge anatoroka na umati wa watu unamfukuza na kumpigia mayowe kuwa ni mwizi. Mwandishi anatueleza katika uk. 132 kuwa *"Kalinge alikimbia kuelekea bwawa kubwa la maji taka…yalitoa povu mfano wa maji ya sabuni…alihisi maisha yake yamo hatarini…alijitosa kwenye bwawa hilo…aliabiri kufa maji."* Kutuhumiwa kuwa mwizi, kufukuzwa na umati unaotishia kumuua na kujitosha kwa bwala la maji taka ni tukio linaloashiria dhuluma ya kisaikolojia. Dhuluma ya kisaikolojia huwa na athari hasi kwa watoto. Kulingana na utafiti wa Gossmann na Fegert (2014) walibaini kuwa watoto waliodhulumiwa kisaikolojia huwa na msongo wa mawazo, hawajiamini na hisia zao hazipo imara.

Ulanguzi wa Watoto na Unyanyasaji wa Kiuchumi

UN (2000) inaeleza ulanguzi wa watoto kama kuwasafirisha, kuwaficha na kuwauza watoto pasi na hiari yao kwa lengo la kuwanyanyasa kiuchumi au kingono. Katika *Kivuli cha Madhila* haki ya watoto ya kulindwa dhidi ya kulanguliwa inakiukwa. Katika uk. 66, Bwana Fedha pamoja na washirika wake wanafanya biashara ya kuwalangua watoto kwa mataifa mengine. Kalinge anaelezewa na Mbanda kuwa baadhi ya watoto wavulana husafirishwa kwenda nchi za ughaibuni kama vile Uarabuni na Pakistan pasi na hiari yao kufanya kazi za forodha, uhamali, ubaharia na kutunza familia za kitajiri. Anazidi kumweleza kuwa wengi wao hufia pale, wengine hutoweka kabisa wazazi wao wasijue kabisa waliko.

Kama kitendo lenye utovu wa maadili, ulanguzi wa watoto huishia katika unyanyasaji wa kiuchumi.

Madhila haya yanaendelezwa pale ambapo watoto kwenye kinu cha pamba wanafanya kazi nyingi na wanalipwa mshahara mdogo sana. Wanafanya kazi siku sita kuanzia saa moja za asubuhi hadi usiku na wanapumzika tu Jumapili (uk. 64). Kipengele cha 32 cha UNCRC (1989) kinaeleza kuwa mtoto anapaswa kulindwa kutokana na unyanyasaji wa kiuchumi ambao unaweza kumdhuru na kushusha hadhi yake. Hali hii ni kinyume katika kinu cha pamba.

Kalinge anashawishiwa kucheza kamari na Saidi na mhudumu wa baa anayeitwa Nakija anayemsihi hivi: *"unataka kucheza game? …vijana kama wewe hujaa tele hapa …waliingia maskini wakatoka matajiri…"* (uk. 73). Katika uk. 74, mwandishi anatueleza kuwa *"Nakija akazidi kumjaza pumzi ya matamanio ya kupata pesa. Ilipofika jioni, Kalinge alikuwa hoi kutokana na utashi mkubwa wa kutaka kujaribu bahati yake…"* Kalinge anakata shauri kucheza kamari na kwa bahati mbaya anapoteza hela zote alizokuwa nazo. Ottisova na wenzake (2018) wanaeleza kuwa ulanguzi wa watoto huathiri afya yao ya kiakili kihasi, husongwa na mawazo, hujidhuru kimwili na kujiua. Dhuluma mbalimbali ambazo watoto wanapitia katika novela hii, inalemaza utekelezaji wa Lengo kumi na sita la Maendeleo Endelevu linaoeleza kuwa kila mtoto anapaswa kulindwa kutokana na unyanyasaji wa kiuchumi, utumwa, ulanguzi wa watoto na dhuluma ya aina yoyote ile.

Matumizi ya Dawa za Kulevya na Unyanyasaji wa Kingono

Kwa mujibu wa WHO (2024) dawa za kulevya ni kemikali ambazo hubadilisha hisia, mienendo, tabia na mawazo ya binadamu anayetumia. John na wenzake (2023) wanaeleza kuwa shinikizo la marika ni sababu mojawapo inayowafanya binadamu kutumia dawa za kulevya. Katika kur. 10-11, Kalinge anashinikizwa na wagema kuonja pombe. Wanamsuta na kumwambia kuwa mwanaume ambaye hanywi pombe ni mjinga. Pia, anashinikizwa na Saidi na Nakija kutumia dawa ya kulevya (shisha) katika uk.77 na anapolemewa na kukohoa, wanamcheka na kumkebehi. Dawa za kulevya kama pombe, 'shisha' humfanya mtu kupotelewa na fahamu, kiasi cha kutojijua au kujiamulia mambo fulani. Kulingana na Steinfeld na Torregrossa (2023), dawa za kulevya huathiri kihasi maendeleo ya akili yao, matokeo yao shuleni huwa duni na wengine huchukulia kuwa uraibu. Katika hali kama hizi, inakuwa rahisi kuwanyanyasa kimapenzi.

Keenan na wenzake (2025) wanaeleza kuwa unyanyasaji wa kingono ni hali ya kumdhalilisha mtu kupitia maneno ya kingono, kumpapasa mwili bila idhini yake au kumwonesha ishara za kingono pasi na hiari yake. Hali hii inajitokeza katika novela ya *Kivuli cha Madhila* pale ambapo Nakija (uk.78) anapapasa mwili wa Kalinge wakiwa wameketi pasi na hiari yake. Hali hii inamchukiza Kalinge na mwandishi anatueleza kuwa *"…aliushika na kuutupa mkono uliokuwa ukiyakagua maungo yake…"* (uk. 79). Matukio haya yanaashiria ukiukaji wa haki za Kalinge kwani kulingana na UNCRC (1989) kipengele cha 33, mtoto anapaswa kulindwa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Kipengele cha 34, kinamhitaji mtoto alindwe kutokana na unyanyasaji wa aina yoyote ya kingono. Hali ambayo Kalinge anapitia inakiuka Lengo la kumi na sita la Maendeleo Endelevu linasema kuwa kufikia mwaka wa 2030, jamii inapaswa kuwa imekomesha unyanyasaji wa kingono kwa watoto na walindwe na jamii kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Briere na wenzake (2024) walibaini katika utafiti wao kuwa watoto walionyanyaswa kingono walikuwa na wasiwasi, msongo wa mawazo na kulikuwepo na uwezekano mkubwa wa wao kunyanyaswa tena kingono kwa sababu waliowanyanyasa walishinikiza kwa vitisho wasiwaambie yeyote kuhusu tendo hilo.

Hitimisho na Mapendekezo

Ukiukaji wa haki za watoto huishia kudumaza rasilmali muhimu inayotegemewa kwa kizazi cha kesho. Watoto wasipopata elimu, lishe bora na matibabu, basi, ukuaji wao utavyazwa na vipawa vyao kukosa kunolewa kwa ajili ya kutumiwa kuzalisha utajiri kwa taifa.

Ili Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu watoto na vijana yaweze kuafikiwa kikamilifu kufikia mwaka wa 2030, pana haja ya wanajamii kuelimishwa na kuhamasishwa kupitia fasihi, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na mifumo mingine namna haki hizo hukiukwa. Pia, pana haja ya wanajamii kuelimishwa namna ya kulinda haki hizo. Ili kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa ajili ya ukuzaji wa maadili na upanuzi wa viwanda, ni muhimu asasi za dola ziwajibikie ulezi na ulinzi wa watoto haki za huku hatua kali za kisheria zikichukuliwa dhidi ya

wanajamii wanaojihusisha na matendo yanayohujumu haki za watoto.

Marejeleo

Alfarhan, I. E. (2024). The influence of Literature on the society. *International Journal of Social Sciences and Humanities Research*. Vol. 12(1), pp. 263-270. https://doi.org/10.5281/zenodo.10886693.

Al-Shuaibi, A. (2014). *The Importance of education*. Doha: Salalah College of Technology.

Aransiola, T.J. & Justus, M. (2018). Child labour hazard on mental health: Evidence from Brazil. JMent Health Policy Econ. Jun 1;21 (2): 49-58. PMID:29961044.

Boehle, J. (2021) Forgiveness, restorative justice and reconciliation in sustainable peacebuilding: Contemporary debates and future possibilities. *Global Change and Security*. Vol. 33 (2), pp. 103-123. https:doi.org/10.1080/14781158.2021.1910226 .

Briere, J. Runtz, M. & Keara, R. (2024). Child and adolescent exposure to sexual harassment: Relationship to Gender, contact sexual abuse and adult psychological symptoms. *Journal of Interpersonal Violence.* Vol. 39, Issue 13-14. https://doi.org/10.1177/08862605231225524.

Cappa, C. (2023). International Classification of violence against children. United Nations Children's fund. https://www.unicef.org/transmonee/media/826/file/2.1%20International%20classification%20of520violence%20against%20children%20.pdf.

Children Act, Cap. 141. (2022). *Kenyan Law.* https://new.kenyalaw.org/akn/ke/act/2022/29/eng%402022-07-29.

Creswell, J. & Poth, C. (2024). *Qualitative inquiry and research design: Choosing among five approaches (15th ed.)* Sage Publications.

Doherty, D. & Berglund, D. (2008). *Psychological abuse: A discussion paper.* Canada: National Clearinghouse on Family Violence.

Ferrara, P., Franceschini, G., Villani, A. & Corsello, G. (2019). Physical, psychological and social impact of school violence on children. *Italian Journal of Pedriatics,* Vol. 45 (1), pp. 46. https://doi.org/10.1186/s13052-019-0669-z.

Frankline, R. Kamin, K. & Russell-Johnson, A. (2026). Counseling clients on disinheritance: Psychological consequences and ethical considerations. *ACTEC Law Journal.* https://doi.org/10.2139/ssrn.6663778.

Gossman, E. Fegert, J. M. Misshandlung, K. & Jugendlichen. (2024). Emotional maltreatment of children and adolescents -Definitions, prevalences, risk factors and psychological consequences. *Jan.* 73 (1) pp. 28-54.

John, M. L., Otene, I. J. J. & Antenyi, G. E. (2023). An overview of drug abuse: Causes, effects and control measures. *Asian Journal of Medicine and Health.* Vol. 21 (11) pp. 263-268.

Kasuma, R. M. & Odawo, M. A. (2025). Udumishaji tabaka kama kichocheo cha ufyefye wa maadili ya kielimu katika riwaya teule za Ken Walibora. Katika M. Kandagor, J. Kobia, I. Mwangi, L. C. Mwita & F. S. Wanjala (Wah.). *Fasihi na masuala ibuka.* Dar es Saalam: TATAKI. Kur. 129-148.

Keenan. C., Masser, B., Neall, A. na Barlow, F. (2025). Recognizing gender harassment in the workplace: A qualitative analysis. *Sex Roles*, *91* (10), Article 67 https://doi.org/10.1007/s11199-025-01617-y.

Kiumi, J. K. & Chiuri, L. W. (2005). *Planning and economics of education*. Nairobi: Pangulin Publisher Limited.

Krippendorff, K. (2018). Content analysis: *An introduction to its methodology* (4th ed.) Sage Publications.

Law of succession Act, Cap. 160 (2015). *Kenyan law.*https://new.kenyalaw.org/akn/ke/act/1972/14.

Meyer, J.W. (1977). The effects of education as an institution. *American Journal Sociology*, Vol. 10.

Momanyi, C. (2023). *Kivuli cha Madhila.* Nairobi: Queenex Publishers Limited.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili: Kozi za fasihi vyuoni na vyuo vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Murimi, J. & Mukuta, J. (2024). Ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya za Kiswahili: Mfano wa *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. *IJO-International Journal of Social Science and Humanities Research.* Juz. 7 (5). Kur. 1-19.

Musindalo, M. A. (2020). *Taswira ya haki za watoto katika riwaya teule za Kiswahili za milenia mpya*. Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu cha Maseno.

Mwita, L. C. & Odawo, M. A. (2020). Tathmini ya lugha ya Kiswahili katika kutimiza Lengo la Maendeleo Endelevu la elimu bora katika nchi za Afrika Mashariki. Katika M. Kandagor (Mh.). *Kiswahili na Maendeleo ya Afrika Mashariki.* Dar es Saalam: TATAKI. Kur. 58-73.

Ndiku, J. M. (2007). The issue of poverty in the provision of quality education in Kenyan secondary schools. *Educational Research and Review*. Vol. 2 (7), pp. 157-164.

Ngatia, R., Njoka, J. N. & Ndegwa, L. (2020). Analysis of corruption risky areas in public secondary school in Nyandarua and Nakuru Counties in Kenya. *American Journal of Humanities and Social Sciences Research*. Vol. 4(4), pp.17-27.

Nussbaum, M. C. (1995). *Poetic justice. The literacy imagination and public life.* Boston: Beacon Press.

Ogechi, N. O. (2024). *Taratibu za kuendesha utafiti na masuala mengine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ogonda, S. S. (2026). Tamthilia za Kiswahili kama chombo cha uhamasishaji kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu: Mifano ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* na *Kodi. Eastern Africa Journal of Kiswahili.* Juz. 5 (1). Kur. 32-41. https://doi.org/10.51317/eajk.v5il.973.

Ottisova, L., Smith, P., Shetty, H., Stahl, D. Downs, J. &Oram, S. (2018). Psychological consequences of child trafficking: An historical cohort study of trafficked children in contact with secondary mental health services. *PLOS ONE, 13(3).*

Plumer, G. & Groake, L. (2011). Cognition of literacy ethical criticism. *OSSA Conference Archive* 22. https://scholar.uwindor.ca/ossaarchive/OSSA9/papersandcommentaries/22.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu*. Dodoma-Tanzania: Central Tanganyika Press.

Posner, R. A. (2009). *Law and literature* (3rd ed.). Cambridge: Harvard University Press.

Schofield, G. & Beek, M. (2025). Providing a secure base: Parenting children in long-term foster family care. *Attachment & uman development.* Vol. 7(1), pp. 3-26 https://doi.org/10.1080/14616730500049019.

Situma, J. & Wasike, M. (2020). The Challenges of examination malpractices in institutions of higher learning in Kenya. *International Journal of Academic Research in Business and Social Sciences*. Vol. 10(9), pp. 699-710.

Steinfeld, M. & Torregrossa, M. M. (2023). Consequences of adolescent drug abuse. *Translational Psychiatry, 13* (313).

The Government of Kenya. (2010). *The constitution.* Nairobi: Government Printers.

Thiele, B. (2002). The human right to adequate housing: A tool for promoting and protecting individual and community health. *American Journal of Public Health.* Vol. 92 (5). Pp.712-715.

UNCRC, (1989). *Convention on the rights of a child*. https://www.ohchr.org/en/instruments-mechanisms/instruments/conventio-rights-child.

UNESCO, (2024). *Culture and Sustainable Development Goals*. UNESCO Publishing.

UNESCO, (2024). *Transforming education towards SDG4: Report of a global survey on country actions to transform education.* https://www.unesco.org/en/articles/transforming-education-towards0sdg4-report-global-survey-country-actions-transform-education.

Ungvarsky, J. (2024). *Wellbeing*. In https://www.ebsco.com/research-starter/health-and-medicine/well-being.

UNHCHR, (2017). *Protecting the rights of the child in humanitarian situations.* https://digitallibrary.un.org/record/3843475.

Received 03/07/2026; Revised 09/08/2026; Accepted 25/09/2026

UNICEF, (2024). *The state of the world's children 2024: The future of childhood in a changing world.* https://www.unicef.org/reports/state-of-worlds.children/2024.

UNICEF, (2024). *Violence against children.* https://www.unicef.org/reports/state-of-worlds.chidren/2024.

UNICEF-WHO, (2020). *Putting children at the centre of the Sustainable Development Goals.* https://www.who.int/publicatins/i/item/putting-children-at-the-centre-of-the-sustainable-develoment-goals.

United Nations Centre for Human Settlements, (1996). *The Habitat Agenda: Goals and principles, commitments and global plan of action.* Nairobi: United Nations.

United Nations, (2000). *Protocol to prevent, suppress and punish trafficking in persons especially women and children, supplementing the United Nations Convention against Trans National Organised Crime.* https://www.unodc/documents/treaties/special/2000%20Protocol%20%to%Prevent,%20Suppress%20and%20Punish%20Trafficking%20in%20persons.pdf.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wangai, M. (2024). Democracy and family wealth regulation in Kenya: A responsive regulation approach to inheritance tax. *King's Law Journal, 35*(1), 89-109. https://doi.org/10.1080/09615768.20.24.2323796. ri

World Health Organisation. (2026, May 7) Violence against children. https://www.who.int/news-room/facts-sheets/detail/violence-against-children.

Ziegler, J. (2001). *The right to food: Report by the Special Rapporteur on the right to food, submitted in accordance with Commission on Human Rights resolution 2000/10* (E/CN.4/2001/53). United Nations Commission on Human Rights.